

HALMASHAURI YA JIJI LA MWANZA

(Barua zote zitumwe kwa Mkurugenzi wa Jiji)

Simu Mkurugenzi : 255(28) 2501375
Ofisi zote : 255 (28) 40334
Fax : 255 (28) 2500785
E-mail. cd@mwanzacc.go.tz
info@mwanzacc.go.tz



S. L.P. 1333
MWANZA.
TANZANIA

Kumb Na. E.30/1/Vol. IX/ 22

3 Novemba, 2017

TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI YA MSIMAMIZI MSAIDIZI WA KITUO NA.1

1. Msimamizi wa Uchaguzi wa Jimbo la **Nyamagana** anatangaza nafasi za kazi ya **MSIMAMIZI MSAIDIZI NA 1 WA KITUO CHA KUPIGIA KURA** ambaye atakuwa na jukumu la kusimamia shughuli za uchaguzi na kuhakikisha utulivu na usalama katika kituo cha kupigia kura kwenye kwenye Uchaguzi wa Marudio Kata ya Mhandu kujaza nafasi Wazi ya Diwani utakaofanyika **tarehe 26 Novemba, 2017.**

Aidha, majukumu mengine ya Msimamizi wa Kituo Na. 1 ni:-

- Kupokea na kutunza vifaa kwa ajili ya Uchaguzi katika kituo,
- Kukagua kadi ya mpiga kura aliyokuja nayo na kuthibitisha kuwa taarifa zake zinalingana na taarifa zilizomo katika Daftari la Wapiga Kura la Kituo,
- *Kusoma kwa sauti jina la mpiga kura aliyekuja Kituoni ili Mawakala wasikie na wantambue,*
- Kuweka alama ya vema (√) kwenye jina la Mpiga Kura lililopo katika Daftari la Wapiga Kura mara baada ya kuthibitisha utambulisho wa Mpiga Kura,
- Kumwelekeza Mpiga Kura kwa Msimamizi wa Kituo ili apatiwe karatasi za kura,
- Atawajibika kwa Msimamizi wa Kituo cha Kupigia Kura.

2. SIFA ZA MSIMAMIZI MSAIDIZI NA 1 WA KITUO CHA KUPIGIA KURA

- Awe raia wa Tanzania,
- *Ikiwezekana* awe mkazi wa Kata ya MHANDU ambayo atafanyia kazi ya kusimamia Upigaji Kura na Kuhesabu Kura,
- Asiwe Kiongozi au Shabiki wa Chama cha Siasa,
- Awe *Mwadilifu, Mvumilivu, Mpole, Mtifu, Msikivu* anayeweza *kufanya kazi kwa kujituma,*

- Awe na elimu ya Kidato cha nne au zaidi na anayeweza kusoma na kuandika vizuri. Pia anayeweza kuyaelewa *Maelekezo ya Wasimamizi wa Vituo vya Kupigia Kura*,
- Awe na uwezo wa kuelewa vizuri Maelekezo ya Tume yanayohusu Orodha ya Wapiga kura,

3. UTARATIBU WA KUOMBA NAFASI YA KAZI

Mwombaji anapaswa kuomba nafasi husika akitoa taarifa kamili zinazomhusu kulingana na sifa zilizotajwa na pia akitaja; kazi yake anayofanya hivi sasa, namba yake ya simu, Jimbo, na Kata anayokaa.

Aidha, Mwombaji ambatanishe picha moja ya rangi yenye ukubwa wa pasi ya kusafiria (passport size), vyeti na kitambulisho chochote alichonacho.

Waombaji walioajiriwa wapitishie maombi yao kwa Waajiri wao.

Maombi yote yatumwe kwa:-

**Msimamizi wa Uchaguzi,
Jimbo la Nyamagana,
S.L.P. 1333
MWANZA**

Maombi ya nafasi ya kazi hii ya Msimamizi wa Kituo cha Kupigia Kura yanaweza kuwasilishwa moja kwa moja katika Ofisi ya Msimamizi wa Uchaguzi, Halmashauri ya Jiji la Mwanza.

4. MUDA WA MWISHO WA KUWASILISHA MAOMBI (DEAD LINE)

Muda wa mwisho wa kuwasilisha Maombi ya nafasi ya kazi ni tarehe 11/11/2017 saa 9:30 Alasiri.

**KIOMONI KIBURWA KIBAMBA
MSIMAMIZI WA UCHAGUZI
JIMBO LA NYAMAGANA**